

UTANGULIZI

Ni Nini? Kusoma pamoja na mtoto wako ni sehemu muhimu ya ukuzi wake wa usomaji. Usomaji wa Majira ya Kiangazi ni fursa ya wanafunzi kuchagua kile wanachotaka kusoma na jinsi wanavyotaka kufanya hivyo.

Epuka "Mteleo wa Kiangazi": Utafiti umeonyesha kwamba wanafunzi ambao hawasomi wakati wa kiangazi wana mwelekeo wa kupoteza kiasi fulani cha ukuzi wa kujifunza ambacho walikuwa wamefikia katika mwaka uliopita wa shule.



TAARIFA KWA FAMILIA

Usomaji wa Majira ya Kiangazi ni fursa ya kumsaidia mtoto wako akuze tamaa ya kudumu ya kupenda kusoma, na wakati ulielele kutegemeza na kuimarisha mafanikio yake ya mwaka wa shule uliotangulia na kumtayarisha kupata mafanikio zaidi wakati wa majira ya kupukutika kwa majani!

Kuanza: Zungumza na mtoto wako kuhusu umuhimu wa usomaji wa majira ya kiangazi!

- Andaa fursa ya kuchagua vitabu vyenye kuvutia zaidi
- Panga wakati hususa wa kusoma
- Nakili muda unaotumika kusoma
- Zungumza na mtoto wako kuhusu kile anachosoma!
- Mtegemeze mtoto wako anapotekeleza usomaji wake

Rasilimali: Madokezo zaidi ya vitabu, miongozo ya wazai, video, fomu za rekodi ya usomaji, na habari nyinginezo zinaweza kupatikana:

- Tovuti ya Usomaji wa Majira ya Kiangazi ya Shule za Umma za Worcester: <http://tinyurl.com/j8om7b2>
- Nje ya Mtandao? **Tembelea Maktaba ya Umma ya Worcester!**

DAKIKA 20 unazotumia ukisoma ndizo sehemu muhimu zaidi ya siku yako!

Chunguza vitabu vilivyoandikwa na waandishi hawa mashuhuri!

Fiction: Speak by Anderson; Beauty Queens by Bray; Hate List by Brown; Fat Angie by Charlton-Trujillo; The Perks of Being a Wallflower by Chbosky; Nick and Norah's Infinite Playlist by Cohn and Levithan; Staying Fat for Sarah Byrnes by Crutcher; Mare's War by Davis; The Living by De la Pena; Born Confused by Desai Hidir; For the Win by Doctorow; The Hazelwood Trilogy by Draper; Keesha's House by Frost; Best of the Best by Green; Crank by Hopkins; The First Part Last by Johnson; Real Time by Kass; Reality Boy by King; Girl in Translation by Kwok; Cut by McCormick; Say What You Will by McGovern; Monster by Myers; Gabi, A Girl in Pieces by Quintero; Buried Onion by Soto; American Born Chinese by Yang

Classic Fiction: Go Ask Alice by Anonymous; A Clockwork Orange by Burgess; The Adventures of Sherlock Holmes by Doyle; Annie on My Mind by Garden; Not Without Laughter by Hughes; Their Eyes Were Watching God by Hurston; Frankenstein by Shelley; Slaughterhouse Five by Vonnegut

Informational Text: Sugar Changed the World by Aronson; Spies of Mississippi by Bowers; We Beat the Street by Davis; Faces from the Past by Deem; Because They Marched by Freedman; Letters to a Young Brother by Harper; We Turned Back to See Where We Came From by Hinojosa; Marvel Comics: An Untold Story by Howe; Flesh and Blood so Cheap: The Triangle Fire and Its Legacy by Marrin; The Other Wes Moore: One Name, Two Fates by Moore; Food Rules: An Eater's Manual; The Immortal Life of Henrietta Lacks by Skloot; Simeon's Story: An Eyewitness Account of Kidnapping of Till by Wright

Mystery and Suspense: Kissed by an Angle by Chandler; The Moonstone by Collins; The Face on the Milk Carton by Cooney; Croak by Damico; Burning Blue by Griffin; Skeleton Crew by King; Bel Canto by Patchett; The Angel Experiment by Patterson; Tokyo Heist by Renn

Science Fiction and Fantasy: The Hitchhiker's Guide to the Galaxy (series) by Adams; Ship Breaker (series) by Bacigalupi; White Cat by Black; Parable of the Sower by Butler; Ready Player One by Cline; Preludes and Nocturnes by Gaiman; Magic's Pawn by Lackey; Proxy (series) by London; The Night Circus by Morgenstern; The Sparrow by Russell; The Scorpio Races by Stiefvater; Leviathan (trilogy) by Westerfeld

Poetry: The Best American Poetry (multiple years) by Doty; The lightning Dreamer by Engle; You Done Even Know Me by Flake; Burned/Smoke by Hopkins; Sold by McCormick; Dizzy in Your Eyes: Poems About Love by Mora; Street Love by Myers; A Fire in my Hands by Soto

Biography and Autobiography: Stronger by Bauman; Zeitoun by Eggers; Zlata's Diary: A Child's Life in Wartime Sarajevo by Filipovic; Look Me in the Eye: My Life with Asperger's by Robinson; Persepolis (graphic series) by Satrapi; I Am Malala by Tausafzai; When I was a Soldier by Zenatti

Advanced Placement: Students who will be taking AP and Honors courses in the next school year should check with their teachers for the required summer reading list and writing activities.



Find more suggestions on the WPS Summer Reading Website:
<http://tinyurl.com/j8om7b2>



Shule za Umma za Worcester ni Taasisi ya Mwajiri/Elimu inayotoa Fursa Sawa / Utetezi wa Wanyonge na haina ubaguzi wa rangi, jinsia, umri, dini, taifa, jinsia, hali ya ndoa, mapendezi ya kingono, ulemavu au kutokuwa na makazi. Shule za Umma za Worcester hutoa fursa sawa ya ajira na programu mbalimbali za elimu, kazini na ufundi. Unaweza kupata habari zaidi zinazohusiana na Fursa Sawa / Utetezi wa Wanyonge kwa kuwasiliana na Meneja wa Rasilimali, 20 Irving Street, Worcester, MA 01609, 508-799-3020.


SHULE ZA UMMA ZA WORCESTER

Matakwa ya Usomaji Majira ya Kiangazi



Wanafunzi Wanaoingia
Darasa la 9 hadi 12

2016



www.worcesterschools.org

HATUA YA 1: Jiwekee LENGU!

Wanafunzi wanaoingia Darasa la 9 hadi 12 watasoma **vitabu vitatu au kurasa 800** wakati wa majira ya kiangazi. Pia, wanafunzi watatimiza migawo **mitatu** kutokana na vitabu walivyosoma.

Majira haya ya kiangazi nitasoma...

Hatua ya 2: Chagua Kitabu!

Naweza kupata wapi kitabu?

Maktaba ya Umma ya Worcester
Maktaba-Gari ya Libby and Lily
Omba madokezo kutoka kwa marafiki!
Programu za Majira ya Kiangazi
Maduka ya Vitabu kama vile Barnes & Noble na Amazon
Goodwill na Salvation Army
Vitabu vya Kielektroniki
Vitabu vya dijitali (CD, MP3)

Angalia jalada la nyuma upate madokezo kadhaa!



7 Bora

Mazoea Mazuri ya Kusoma

Unganisha: Ninaposoma nawaza “Hilo lanikumbusha...”

Piga Picha Akilini: Ninaposoma “Naona akilini...”

Rejelea: Ijapokuwa haikusemwa kwenye kitabu, ninaposoma “najua...” “nafikiri...” au “nakisia kwamba...” au “natabiri...”

Tafuta Maana: Ninapochanganyikiwa ninaposoma “Naweza...” Na “Acha nijikumbushe ninachojua...”

Changanua Umuhimu: Ninaposoma “Najua habari nilizosoma ni muhimu kwa sababu...”

Tafakari: Ninaposoma naona mambo yanahusiana nami “najua ni wazo kubwa kwa sababu...” au “Aha...”

Uliza: Ninaposoma, najiuliza maswali kuhusu kitabu ninachosoma kama vile “Huenda ni kwa nini...” au “Nina hamu ya kujua...”

Tambua na Uzingatie

Tua ujulize...

Vinyume na Hali Zinazopingana: Mhusika anaposema au kutenda jambo ambalo ni kinyume (linapingana) na kila unachotarajia afanye jiulize, “Kwa nini mhusika huyu anatenda hivi?” Hilo linaweza kukusaidia kutabiri au kufikia mkataa kuhusu maudhui na mkinzano.

Tena na Tena: Unapooona neno, msemu, kitu, au hali inapotajwa tena na tena, jiulize, “Kwa nini hili linajitokeza tena na tena?” Hilo litakusaidia kuelewa maudhui na mkinzano, au huenda ni ishara ya litakalotokea baadaye.

Pindi ya Kumbukumbu: Mwandishi anapokatiza masimulizi kwa kurudia mambo ya wakati uliopita na kukuambia kumbukumbu fulani, jiulize, “Kwa nini kumbukumbu hiyo ni muhimu?” Hilo litakuambia kuhusu maudhui, mkinzano, na laweza kuwa ishara ya litakalotokea baadaye.

Pindi ya Aha: Mhusika anapotambua, anapoelewa, au kutegua kitendawili, jiulize, “Hilo laweza kubadili mambo jinsi gani?” Ikiwa mhusika ametatua tatizo umegundua mkinzano, ikiwa mhusika amejifunza fundisho la maisha, umegundua maudhui.

Maneno ya Hekima: Mhusika anapomchukua kando mhusika mkuu na kumpa ushauri, jiulize, “Fundisho ni nini, na hilo linaweza kumwathiri mhusika huyo jinsi gani?” Hata fundisho liwe hini, inawezekana umepata maudhui ya masimulizi hayo.

Maswali Magumu: Mhusika anapojiuliza swali gumu, jiulize, “Swali hilo linanifanya nijiulize nini?” Hilo litakusaidia kutabiri yatakayotokea.

(Habari hizi zinategemea chapisho Notice and Note lililoandikwa na Kylene Beers.)

Hatua ya 3: Soma, Soma, SOMA!

Starehe, furahia kusoma kitabu kizuri, uwe na wakati mzuri! Fikia malengo yako: Naweza kusoma wapi? Naweza kusoma wakati gani? Ni nini ninachopenda katika hadithi? Kumbuka, ikiwa ni kitabu kizuri, mpendekezee rafiki yako!



Hatua ya 4: Timiza Mgawo!

Timiza migawo ifuatayo. Chaguo ni lako, furahia kueleza ulichosoma! **Migawo ya kusoma ya majira ya kiangazi ni asilimia 10 ya maksi za muhula wa kwanza!**

Taarifa: Wanafunzi watakoafanya mitaala ya AP katika mwaka ujao wa shule wanapaswa kuwasiliana na walimu wao wa AP ili kujua migawo yao ya kusoma na kuandika wakati wa majira ya kiangazi.

Kitabu cha Kwanza: Shajara Maradufu

Jaza shajara maradufu. Unaweza kupata fomu kwenye tovuti ya Usomaji wa Majira ya Kiangazi ya Shule za Umma za Worcester.


Kitabu cha Pili: Linganisha na Kutofautisha

Linganisha au utofautishe habari hii na nyingine ambayo umesoma. Andaa habari kutokana na usomaji wako zinazounga mkono madai yako.

Kitabu cha Tatu: Chaguo ni Lako! (Chagua Moja)

Timiza mradi mmoja kuhusu kitabu ulichosoma kama vile kuandika shairi, hati ya tamthilia, mchono wenye maelezo, picha yenye maelezo, au video.

Tembelea tovuti ya Usomaji wa Majira ya Kiangazi ya Shule za Umma za Worcester ili upate madokezo zaidi! (<http://tinyurl.com/j8om7b2>)



Unaposoma, usisahau kujiuliza...

Nani, Nini, Wapi, Wakati Gani, Kwa Nini, na Jinsi Gani

Kuwa tayari KUSHEREHEKEA!

Kumbuka kuleta kazi zote ulizotimiza ili mwalimu wako mpya na wanafunzi Wazione siku ya kwanza ya shule!